JINA LA MTAHINIWA ………………………………………………. ………………………………JINA LA SHULE………………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KILIMANJARO**

**MTIHANI WA MHULA WA II – DARASA LA 5**

**01**

**KISWAHILI**

**Muda: Saa 1:30** **Novemba 2024**

## MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **sita (6)**
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika majibu kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au nyeusi
4. Hairuhusiwi kuingia ***na daftari au kitabu*** ndani ya chumba cha mtihani

## SEHEMU A: alama 20

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Sikiliza kwa makini habari utakayosomewa na msimamizi, Kisha jibu kipengele cha (I)- (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika mabano.

i. Ni kiongozi gani aliwatembelea wanakijiji wa Kazamwendo?

A. Mkuu wa wilaya
B. Mwenyekiti wa Kijiji
C. Mkuu wa mkoa.
D. Mwenyekiti wa kitongoji
E. Wanakijiji wa Kazamwendo

ii. Uchaguzi wa serikali za mitaa hufanyika Kila baada ya miaka mingapi?

A. 4
B. 3.
C. 2.
D. 10
E. 5.

iii. Kutokana na habari uliyosomewa ni viongozi gani huchaguliwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa?

A. Wenyeviti wa vijiji na vitongoji

B. Wakuu wa mikoa

C. Madiwani wa kata

D.Wabunge wa majimbo

E. Rais wa Tanzania.

iv Maneno**"Shangwe na Nderemo"**kama yalivyotumika kwenye habari Yana maana gani?

A. Huzuni.

B. Fujo

C. Furaha

D. Kimyakimya

E. Unyenyekevu

v. Ni Kijiji gani kilitembelewa na mkuu wa mkoa

A. Gezaulole.

B. Kazamwendo

C. Songwe

D. Mtakuja

E. Utakuja

2. Katika kipengele cha (I) - (v) chagua jibu sahihi Kisha andika herufi yake katika mabano uliyopewa

i. Hakuna mtu ......... aliyebisha hodi.

A. yoyote

B. wowote

C. zozote

D. yeyote

E. wote

ii. Kauli taarifa ya sentensi " Soma kwa bidii" , Baba aliniambia. ni

A. Baba aliniambia kuwa nisome kwa bidii

B. Baba alimwambia kuwa asome kwa bidii

C. Baba aliniambia nisome kwa bidii

D. Aliniambia baba nisome kwa bidii

E. Baba alisema nisome kwa bidii

iii. ........ni  mbuzi wa mzee Chapakazi

A. hizi.

B. hii

C. hivi

D. hayo

E. hawa

iv. Atasafiri keshokutwa . Kiambishi Cha wakati ni kipi?

A. a

B. sa

C. ri

D. ta

E. fi

v. Kinyume Cha neno **Shaibu** ni .....

A. Binti

B. Barubaru.

C. Mwanaume

D. Mzee

E. Kikongwe

vi. Nilipofika Arusha nilipata ........ wa kutembelea mbuga za wanyama.

A. tunu.

B. Nusra

C. Msimu

D. Ruhusa

E. Wasaa

Vii. Angelisikiliza maelekezo vizuri......... mtihani.

A. asingelifaulu

B. angalifaulu

C angelifaulu

D. angepasi

E. asingalifaulu

viii. Neno **abadani** lina maana gani?

A. Angalau.

B. Ndio

C.kamwe

D. Ndani

E. sawa

ix. Tunasafiri ......... garimoshi kwenda Dodoma.

A. kwa

B. Bila

C. na

D. si

E. pamoja na

x. Bahati ana Ukwasi wa Ng'ombe wa maziwa . Ni neno gani lenye maana sawa na **Ukwasi**?.

A.umasikini

B. Utajiri

C. Majivuno

D. hodari

E. utaalamu

**2. Majibu**

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

3. Oanisha vitendawili, Methali na Nahau zilizopo kwenye **orodha A** na majibu yake kutoka **Orodha B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika nafasi ya majibu

| **Na.** | **Orodha A** | **Majibu** | **Orodha B** |
|---|---|---|---|
| I. | Fua dafu | ( ) | A. Si mtoro |
| ii. | Wali wa mama mtamu | ( ) | B. Nazi |
| iii. | Mwenda kwao | ( ) | C. Kuwa na kiburi |
| iv. | Pata kichwa | ( ) | D. Kibatari |
| v. | Jini mnywa damu haangazi bila damu | ( ) | E.hutunzwa |
| | | | F.weza jambo |
| | | | G. Usingizi |

**SEHEMU B : alama 10**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

4. Soma shairi lifuatalo Kisha jibu maswali ya kipengele (I) - ( v) **kwa kuandika jibu sehemu iliyoachwa wazi**

Kiswahili naazimu, sifayo inayokabwa

Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa

Toka kama chemchemu, furika palipozibwa

Titi la mama ni tamu, jingine halishi hamu.

Kiswahili ni tajiri, kwa fasaha na Methali

Na mimi ninafikiri, kimeshafika mbali

Kimeweza kusafiri, taaluma mbalimbali

Titi la mama ni tamu, jingine halishi hamu.

Maswali

I. Shairi hili lina beti ngapi?................,..........................................................................................................................................

ii. Taja vina vya kati na vya mwisho katika Ubeti wa mwisho........................................................................

iii. Taja kituo Cha shairi hili ..................................................................................................................

iv. Shairi hili lina mizani ngapi? ..........................................................................................................

v. Andika kichwa Cha shairi hili...................................................................................................................

**SEHEMU C : alama 10**

**5.** Jibu kipengele cha ( I) - (v) **kwa kuandika vipengele vya barua ya kiofisi**

| . |
|---|

| ii. |
|---|

| iii. |
|---|

| iv. |
|---|

| Kiini cha barua |
|---|

| Mwisho wa barua |
|---|

| v. |
|---|

**SEHEMU D: alama 10**

**6**. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko mzuri kwa kuzipa herufi **A, B, C, D na E** ili zilete mtiririko mzuri.

i. Niliogopa lakini nilipiga moyo konde …………………………………………………………………………..

ii. Jumamosi iliyopita mama aliniagiza sokoni…………………………………………………………………….

iii. Nilirudi nyuma kidogo nikaokota fimbo na kumpiga Yule nyoka mpaka akafa……………………………

iv. Nilipokuwa njiani nilimuona nyoka……………………………………………………………………………........................................

v. Aliniagiza nikanunue nyama, vitunguu, sukari, mchele na mafuta ya kupikia……………………………….

**JINA LA MTAHINIWA ……………………………………………… …………………………….JINA LA SHULE………………………………**

**MAJIBU**

**SEHEMU A. Alama 20 @ swali 1**

1. i. C

ii. E

iii. A

iv. C

v. B

2.

i. D

ii. A

iii. E

iv. D

v. B

vi E

vii. C

Viii. C

ix. A

x. B

3.

i. F

ii. G

iii. A

iv. C

v. D

**SEHEMU B.Alama 10 swali@2**

i. Mbili

ii. **ri** na **li**

iii. Titi la mama ni tamu, jingine halishi hamu.

iv. 128

v. Lugha ya Kiswahili

**SEHEMU C : alama 10@ swali 2**

**i.** anuani ya mwandishi

ii. tarehe

iii. Anuani ya mwandikiwa

iv. Kichwa cha barua

v. saini na jina la mwandishi

**SEHEMU 2 :Alama 10@ swali 2**

i. D

ii.A

iii. E

iv.C

v.B

**JINA LA MTAHINIWA ……………………………………………. ……………………………JINA LA SHULE………………………………**

# UFAHAMU WA KUSIKILIZA

Siku moja mkuu wa mkoa wa Songwe aliwatembelea wananchi wa Kijiji cha Kazamwendo. Baada ya kuwasili kijijini hapo alipokelewa kwa **shangwe na nderemo** na mkuu wa wilaya pamoja na wanakijiji. Katika hotuba ya mkuu wa mkoa aliwasisitiza wananchi wa kijiji cha kazamwendo kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa;  ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano. Aidha , aliwaeleza wanakijiji kuwa uchaguzi huo ni kwa ajili ya kuwapata wenyeviti wa vijiji na vitongoji. Kwani kwakufanya hivyo kutasaidia kupata viongozi watakaoleta maendeleo kwa wananchi.

Siku moja mkuu wa mkoa wa Songwe aliwatembelea wananchi wa Kijiji cha Kazamwendo. Baada ya kuwasili kijijini hapo alipokelewa kwa **shangwe na nderemo** na mkuu wa wilaya pamoja na wanakijiji. Katika hotuba ya mkuu wa mkoa aliwasisitiza wananchi wa kijiji cha kazamwendo kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa;  ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano. Aidha , aliwaeleza wanakijiji kuwa uchaguzi huo ni kwa ajili ya kuwapata wenyeviti wa vijiji na vitongoji. Kwani kwakufanya hivyo kutasaidia kupata viongozi watakaoleta maendeleo kwa wananchi.

Siku moja mkuu wa mkoa wa Songwe aliwatembelea wananchi wa Kijiji cha Kazamwendo. Baada ya kuwasili kijijini hapo alipokelewa kwa **shangwe na nderemo** na mkuu wa wilaya pamoja na wanakijiji. Katika hotuba ya mkuu wa mkoa aliwasisitiza wananchi wa kijiji cha kazamwendo kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa;  ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano. Aidha , aliwaeleza wanakijiji kuwa uchaguzi huo ni kwa ajili ya kuwapata wenyeviti wa vijiji na vitongoji. Kwani kwakufanya hivyo kutasaidia kupata viongozi watakaoleta maendeleo kwa wananchi.

Siku moja mkuu wa mkoa wa Songwe aliwatembelea wananchi wa Kijiji cha Kazamwendo. Baada ya kuwasili kijijini hapo alipokelewa kwa **shangwe na nderemo** na mkuu wa wilaya pamoja na wanakijiji. Katika hotuba ya mkuu wa mkoa aliwasisitiza wananchi wa kijiji cha kazamwendo kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi wa serikali za mitaa;  ambao hufanyika kila baada ya miaka mitano. Aidha , aliwaeleza wanakijiji kuwa uchaguzi huo ni kwa ajili ya kuwapata wenyeviti wa vijiji na vitongoji. Kwani kwakufanya hivyo kutasaidia kupata viongozi watakaoleta maendeleo kwa wananchi.